



KENYA REVENUE
AUTHORITY



KUELEWA
HUDUMA YA
USHURU KIDIJITALI

Kuelewa Huduma ya Ushuru Kidijitali

1. Ni nini Huduma ya Ushuru Kidijitali (DST)?

Huu ni ushuru unaolipwa kutokana na mapato yaliyopatikana au kuongezeka Kenya kutokana na huduma. Ushuru huu unatolewa kupitia soko la kidijitali.

2. Soko la Kidijitali ni nini?

Soko la Kidijitali ni jukwaa linaloweza mtagusano wa moja kwa moja kati ya wanunuzi na wauzaji wa bidhaa na huduma kupitia njia za kieletroniki.

3. Huduma ya Ushuru Kidijitali (DST) itaanza kutumika lini?

Huduma ya Ushuru Kidijitali iliingizwa katika Sheria ya Fedha ya 2020 na ilianza kutumika tarehe 1 Januari 2021.

4. Ni kipi kiwango cha Huduma ya Ushuru Kidijitali?

Kiwango cha Huduma ya Ushuru Kidijitali ni asilimia 1.5% ya thamani ya mapatano kwa jumla na kinalipwa wakati mtoa huduma anapolipwa kwa ajili ya kutoa huduma.

5. Je, Huduma ya Ushuru Kidijitali ni ushuru wa mwisho?

Kwa wakaazi na makampuni yenye makao ya kudumu Kenya, Huduma ya Ushuru Kidijitali itakuwa ni ushuru unaotokana na kiwango cha mapato yanayotakiwa kulipwa kukidhia ushuru wa mapato katika kipindi cha mwaka kifedha.

Kwa wasiowakaazi na makampuni yasiyo na makao ya kudumu Kenya, Huduma ya Ushuru Kidijitali itakuwa ni ushuru wa mwisho.

6. Nini maana ya Mkaazi?

Kwa ajili ya ushuru, mkaazi ni:

- Mtu binafsi/chombo/shirika lililona makao ya kudumu Kenya na lilikuwapo katika kipindi cha mwaka ambao mapato yanakaguliwa.
- Mtu binafsi ambaye hana makao ya kudumu Kenya lakini amekuwa nchini kwa siku 183 au zaidi katika mwaka wa mapato unaokaguliwa.
- Mtu binafsi ambaye hana makao ya kudumu Kenya lakini amekuwa Kenya kwa wastani wa siku 122 katika mwaka wa mapato unaokaguliwa na miaka miwili mengine ya kuongoza.

7. Nini maana ya Makao ya kudumu?

Aidha, kampuni inaweza kuchukuliwa kuwa na makao ya kudumu Kenya ikiwa:

- Kampuni imesajiliwa chini ya sheria za Kenya.
- Katibu wa Baraza la Mawaziri wa Fedha na Mipango atatoa tangazo kuwa kampuni hiyo imesajiliwa nchini.
- Usimamizi wa kampuni hiyo upo Kenya.

8. Mamlaka ya Mapato Kenya hukusanya vipi Ushuru wa Huduma Kidijitali?

Mamlaka ya Mapato Kenya, itakusanya ushuru wa huduma kidijitali kwa kutumia njia sahali za kujitathmini mwenyewe ambapo mhudumu wa Huduma Kidijitali atatuma/atalipa ushuru.

9. Makampuni ambayo yapo ng'ambo na hayana ofisi zao nchini lakini yanajishughulisha katika soko la kidijitali yatathibitishaje Ushuru wa Huduma Kidijitali?

Kampuni hizo zitahitajika kujisajili, kufaili na kutuma/kulipa ushuru kupitia mfumo sahali wa kujisajili. Aidha, makampuni yanaweza kuchagua mwakilishi wa ushuru ili athibitishie na atume/alipe kodi kwa niaba yao.

10. Je, Ushuru wa Huduma Kidijitali unamaana kuwa makampuni ambayo hayana makao ya kudumu Kenya hutozwa ushuru mara mbili?

Kuanzishwa kwa Huduma ya Ushuru Kidijitali haimaanishi kuwa kutakuwa na utozaji ushuru mara mbili. Kisheria ushuru hutozwa katika nchi ambapo mapato ni chanzi au hupatikana. Kwa mfano, ikiwa kampuni A inauza bidhaa au huduma Kenya, ushuru utalipwa Kenya ambapo mapato yanapatikana.

11. Huduma ya Ushuru Kidijitali una manufaa gani?

- Inahakikisha usawa kwa wahudumu wa Kenya wanaotoa huduma ya kidijitali.
- Inapanua njia za ukusanyaji ushuru.
- Inasababisha kuongezeka kwa ukusanyaji ushuru.



KENYA REVENUE
AUTHORITY

TAX



Tel: +254 (020) 4 999 999, +254 (0711) 099 999 | Email: callcentre@kra.go.ke



www.kra.go.ke



@KRACare



Kenya Revenue Authority



Kenya Revenue Authority

Tuliye Ushuru, Tujitegemee!